# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA TATU

### Kikao cha Tatu – Tarehe 1 Aprili, 2021

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Natoa nafasi kwa Waheshimiwa Wabunge wanaoingia wapate kuingia haraka haraka. Ahsante sana, sasa Katibu.

**NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:**

### KIAPO CHA UAMINIFU

1. Mhe. Balozi Mbarouk Nassor Mbarouk;
2. Mhe. Balozi Liberata Rutageruka Mulamula;
3. Mhe. Balozi Dkt. Bashiru Ally Kakurwa.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa ajili ya kumbukumbu za *Hansard* naomba tusikilizane na hasa hapa.

Kwa ajili ya kumbukumbu za *Hansard* kwa zoezi ambalo limemalizika sasa, ni kwamba nimepata barua ya Mheshimiwa Rais sasa kwa ajili ya *Hansard* kwa zoezi hili ambalo tumelimaliza hivi sasa niseme imeandikwaje. Lakini inahusu uteuzi wa Wabunge watatu katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Imeandikwa kwamba;

Mheshimiwa Spika,

Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya 66(1)(e) Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amepewa mamlaka ya kuteua Wabunge wasiozidi kumi kutoka miongoni mwa watu wenye sifa stahiki za kuwa Wabunge.

Kwa muktadha, huo napenda kutaarifu kwamba nimeteua wafuatao kuwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania:-

1. Balozi Dkt. Bashiru Ally Kakurwa;
2. Balozi Mbarouk Nassor Mbarouk; na
3. Balozi Liberata Rutageruka Mulamula.

Nakutakia majukumu mema.

Mungu Ibariki Tanzania.

Imesainiwa na Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan.

Nashukuru kwamba tumekwishaifanyia kazi maelekezo haya na kwa hiyo, basi nichukue nafasi hii kuwapongeza sana Wabunge wapya waliojiunga pamoja nasi; Mheshimiwa Balozi Mulamula karibu sana. Sisi wenzako tuko hapa tayari, basi tutakupa kila aina ya ushirikiano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Balozi Mbarouk, rafiki yetu kwa wale tuliokuwa tukisafiri mara kwa mara pale Dubai, kwa mara ya mwisho alikuwa Doha pale. Mara nyingi akija kutupokea, kutuaga tukirudi nyumbani, mtu mwema sana huyu. Ahsante sana, tutaku-*miss* Dubai pale. *(Makofi)*

Lakini pia, Mheshimiwa Bashiru Ally Kakurwa, karibu sana mjengoni karibu sana. Kwa niaba ya Wabunge wote nakukaribisheni, nyote watatu. Karibuni sana. *(Makofi)*

Lakini pia nichukue fursa hii kuwapongeza sana, jana tulienda Ikulu pale Chamwino kwa ajili ya uapisho wa Mheshimiwa Makamu wa Rais, Dkt. Philip Mpango, lakini kufika pale kukawa na yatokanayo. *(Kicheko)*

Kutokana na yatokanayo, tumeshindwa kuwa na kipindi cha maswali leo asubuhi kama ilivyo ada kwa sababu ya *shakeup* imekuwa kidogo, inabidi watu wapate nafasi, wakaape, wakabidhiwe Wizara, halafu tuendelee na maswali kama kawaida. Tumeona itatupa shida kidogo kwa siku ya leo, kwa hiyo, leo ilikuwa ni siku ya maswali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, vile vile tukaona haitakaa sawa. Kwa hiyo, leo hakutakuwa na kipindi kwa maswali baada ya kumaliza mimi kusimama hapa, labda nitatoa nafasi kama kuna mwongozo, kuna nini, *otherwise* tutaahirisha shughuli zetu. Niwapongeze sana Waheshimiwa Mawaziri wetu na Naibu Mawaziri wote. *(Makofi)*

Kwanza kwa kubaki kwenye Baraza na huo ndio uzuri wa mama, kabisa amekuwa *very considerate* na huo ndio ukweli jamani,wangekuwa wenzetu wengine hapa upewe panga hilo lalalaaa! Majeruhi yangekuwa kibao, lakini mama aaaah! Kapita salama katikati. Kwa hiyo, sisi kama Wabunge kweli tunamshukuru sana Rais wetu mpendwa tukiamini kwamba dhamana hii ambayo Waheshimiwa Mawaziri mmeipata, mtaifanyia kazi kwa imani ile ile ambayo Mheshimiwa Rais amewapatia. *(Makofi)*

Yako mambo mengi sana ya kufanya, kila mmoja kwenye Wizara yake, na mengi sana mtayapata kama ushauri kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge. Cha msingi Waheshimiwa Mawaziri ninyi ni Wabunge kama sisi. Yaani hapa Bungeni ndio nyumbani, huko mmekwenda matembezi tu, *krikikriki* unarudi hapa. *(Kicheko/Makofi)*

Kwa hiyo, tusisahauliane sana yaani ile! Yaah! Mtapata ushauri mwingi huko Serikalini na kadhalika, lakini msisahau kwamba ushauri wa Wabunge ni ushauri muhimu sana. Kwa sababu ni ushauri wa wananchi kabisa kabisa.

Na kila Wizara ina mambo fulani fulani ya msingi ya kushughulikia. *(Kicheko/Makofi)*

Kwa mfano, mnasikia kila siku habari za wafanyabiashara wa nchi hii wakilalamika, kila siku, hivi Waziri wa Uwekezaji, wa Viwanda na Biashara, wa Fedha na wanaoendana na hiyo kada ya biashara, unahitaji kengele gani igongwe kusema kwamba hili eneo ni kipaumbele namba moja? *(Makofi)*

Waziri wa TAMISEMI, ndio maendeleo ya mwananchi wa kawaida kule vijijini tunakoishi yaani ndio anayewagusa wale wananchi kabisa, yale madarasa yanayojengwa kuwatoa watoto kutokusoma kwenye mti sasa wanasoma kwenye darasa. Wanaacha kukaa chini, sasa wanapata madawati, ile ni thawabu kubwa sana kwa Mwenyezi Mungu. *(Makofi)*

Pamoja na miradi mikubwa tunayoifanya, kielelezo na kadhalika, lakini TAMISEMI ile zahanati, maji, darasa, barabara zao na kadhalika, ni jambo la thawabu kubwa sana, tusiwasahau watu hawa. Hawa wanaoitwa wanyonge TAMISEMI ndio mama yao, ndio baba yao, madawa hakuna. Afya hatumlaumu Waziri wala nini, lakini ndio pa kushughulikia.

Tungekuwa na takwimu halisi wangapi wanapoteza maisha kwa sababu ya hili jambo la dawa, sio jambo la jana wala la juzi, la siku nyingi kila tukikaa *MSD, MSD, MSD* kila mwaka. Hivi kwa nini Wizara ya Fedha msichukue hilo deni la *MSD* ninyi kwani si mna madeni mengi tu mnachukuaga ninyi, kwa nini msichukue hilo deni la *MSD* ili sasa fedha zinazopelekwa *MSD* zitoe dawa na ninyi mtajuana na *MSD* huko kiaina yenu, kila mwaka *MSD, MSD, MSD what is this,* yaani yako kila Wizara kuna mambo ambayo lazima tusonge mbele, lazima tutoke pale.

Tulisema Bima ya Afya kwa Watanzania wote, miaka mitano ikashindikana iliyopita, tumepigwa kwenye kampeni weee! Tumerudi, sasa hilo nalo linahitaji nini? Lazima tuanze

nalo yaani mimi kila Wizara nina maelezo kwa sababu tunaishi huko kwa wananchi tunajua kipaumbele kikubwa ni nini. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tukajitahidi sana tuwatendee haki Watanzania hawa na tumsaidie Rais wetu ambaye ametupa imani kubwa ya sisi kushika bendera pamoja naye ya kuongoza Serikali na sisi kwa sababu sisi ni wenzenu, tutawashauri kwa moyo mweupe, usichukulie kama ni *personal* au ni nini hapana, ni kwa nia njema tu ya kusonga mbele.

Ardhi, tumesema mara nyingi hapa, tukiweza kuipima ardhi yetu yote, mapato yatokanayo na hati za ardhi yanaweza yakai-*double* hii bajeti yetu. Kwa hiyo, badala ya kuajiri sijui manani nani, tuajiri watu wa ardhi, wapima ardhi na wengine tuajiri, kila Wilaya wawe wengi, watu wapimiwe wawe na hati zao. Wenzetu wanaotamba tamba huko wanajifanya wana bajeti kubwa, hela nyingi wanatoa kwenye ardhi, kwa sababu ardhi imepimwa. Yaani yako mambo ambayo katika michango ya Wabunge hapa, tukiichukulia vizuri tukaiweka sawasawa, tunaweza kabisa kumsaidia Rais wetu na tukaisaidia nchi yetu kwa kiwango kikubwa sana. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tunakupongezeni sana, na kwa kweli tunawatakia kila la heri, tunawapenda na Mheshimiwa Waziri Mkuu sisi tutakusaidieni sana kabisa kabisa kuona kwamba mafanikio yanakuwa makubwa kupitiliza.

Basi baada ya matangazo hayo, nikae kwa dakika mbili endapo kuna mwongozo, kuna nini, kuna nini, niseme ya mwisho kama hakuna ninyanyuke niendelee na ya kwangu.

Aaah! Safi inaelekea hakuna. Sasa kuanzia kesho, kama mnavyofahamu kesho ni Ijumaa Kuu.

Waheshimiwa kuna kibunda kiliokotwa pale kwenye *security check*, kiko hapa kwa Makatibu hapa mezani,

sitasema ni kiasi gani ili ukija inabidi useme ni kiasi gani Katibu ukae nayo hiyo, wamedondosha kwenye mashine pale. *(Kicheko)*

Kesho ni Ijumaa Kuu, Ijumaa tunawatakia kila la kheri, kwa sikukuu hii muhimu katika dini ya Kikristo ya Pasaka, Jumamosi, Jumapili, Jumatatu ni Jumatatu ya Pasaka, siku ya Jumanne ni siku ya kazi. Kwa hiyo, tutakuja hapa kama kawaida, tutakuwa na kipindi cha maswali, Waheshimiwa Mawaziri watakuwa wameshakabidhiana ofisi, wameshaweza kuelewa nini ni nini, wanaweza kujibu maswali *by* Jumanne. Wao itabidi wasiwe na Pasaka hapa katikati, hasa wale waliohama Wizara.

Halafu Jumatano, ni *Karume day,* sasa kwa jinsi ambavyo mambo yamekuwa, ratiba yetu ya Bunge imekuwa ime-*shake shake* sana, kwa hiyo, tumeomba siku ya *Karume day* mchana, ndio tukutane Kamati ya Uongozi, Kamati ya Bajeti na Serikali. Mheshimiwa Waziri Mkuu tutakuomba siku hiyo na kama ukiwa na nafasi na Waheshimiwa Mawaziri wa zile sekta ambazo tutakuwa tunaziongelea siku hiyo. Tayari jana tulishapeana maeneo muhimu, yenye kipaumbele basi siku hiyo ya *Karume day* Jumatano mchana, saa nane.

Kwa upande wa Kamati ya Bajeti, ilikuwa mkutane leo, haitawezekana sababu Waziri wa Fedha hajaapishwa bado, inabidi jioni hii aende Chamwino kule na wenzake kwenda kupata sasa *instrument.* Kwa hiyo, yale mashauriano ambayo mlikuwa mfanye kati ya Kamati ya Bajeti na Serikali itabidi mfanye siku ya Jumanne tarehe 6 Aprili, 2021 mara baada ya kipindi cha maswali, Kamati ya Bajeti na Serikali. Mkishafanya Jumanne sasa Jumatano saa nane ndio na sisi tunakutana Kamati ya Uongozi, Kamati ya Bajeti na Serikali ili kuweka mambo yote sawasawa.

Eeh na mkumbuke Waheshimiwa Wenyeviti wa Kamati zetu zote hiyo siku ya Jumanne wakati Kamati ya Bajeti inapokutana na Serikali, kufuatana na Kanuni zetu Wenyeviti wote wa kamati mbalimbali ni Wajumbe wa Kamati ya Bajeti siku hiyo. Kwa hiyo, inakuwa Kamati ya Bajeti ile kama ilivyo

lakini Wenyeviti wote wanahudhuria kama Wajumbe wa Kamati ya Bajeti pia ili kuweka mambo haya sawa sawa.

Vinginevyo kwa wale watakaosafiri, kwa kweli nawatakia kila la heri, mjitahidi sana madereva wenu wasikimbie, barabarani na magari, lazima um-*control* dereva. Ushauri wangu gari ikikimbia mwisho kilometa 90 kwa saa inatosha. Ikishafika kilometa 90 unamkumbusha anza kurudi chini kwani mnakimbilia wapi, siku hizi barabara yamekuwa safi, Serikali yetu imefanya kazi kubwa sana, utafika tu, taratibu utafika. *(Makofi/Kicheko)*

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Balozi Liberata Rutageruka Mulamula, ambao ni Dkt. George Mulamula mume wake, oooh! Yule pale, eeeh! Karibu sana shemeji Eeeh mama amekuja na baba kabisa *day one*, jambo zuri sana. *(Kicheko/Makofi)*

Lakini pia yupo Ndugu Luminata Mayerere ambaye ni pacha wa Mheshimiwa Waziri Mulamula, yuko wapi eee huyu huku. Ahsante sana, ahsante sana, karibu sana na Ndugu Michael Mayerere, mume wa pacha, ahsante sana karibuni sana. *(Makofi)*

Lakini wako wageni watatu wa Mheshimiwa Mbarouk Nassor Mbarouk ambao ni Ndugu Raiyan Kassim Mohamed, huyu ni shemeji yetu, mke wake na Mheshimiwa Mbarouk, karibu sana mama karibu sana. Yuko Ndugu Munir Mbarouk, mtoto wake, karibu sana Munir, yuko Amira Mbarouk karibu sana, na yuko Aklam Mbarouk karibu sana karibuni sana, karibuni sana. *(Makofi)*

Kama tunavyofahamu leo saa tisa kamili jioni, zoezi la uapisho litaanza kule Chamwino Ikulu leo, Wenyeviti wote wa Kamati zote na Makamu Wenyeviti wote wamealikwa kwa niaba yetu sisi kuhudhuria hafla hiyo ya uapishwaji wa Waheshimiwa Mawaziri, kwa hiyo, basi la kwenda huko au mabasi ya kwenda huko yataondoka, hapa saa saba kamili juu ya alama mchana, kwa hiyo, naomba sana Wenyeviti na Makamu Wenyeviti tutumie usafiri huo ili tuweze kuwahi

kufika kule mapema. Saa saba kamili juu ya alama mabasi yataondoka katika eneo hili la Bunge.

Kwa kuwa shughuli za leo zimekamilika zote nichukue nafasi hii basi, kuahirisha shughuli za Bunge hadi Jumanne ijayo tarehe 6 Aprili, 2021 saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 03.27 Asubuhi Bunge liliahirishwa hadi siku ya Jumanne, Tarehe 6 Aprili, 2021 Saa Tatu Asubuhi)*